18. THE TIME MACHINE

18. THE TIME MACHINE

Karibu kwenye muhtasari wa kitabu cha KUMI NA NANE kwenye orodha ya vitabu 100 ninavyosoma kwa siku 100.
THE TIME MACHINE ni riwaya iliyoandikwa na H. G. WELLS, inayohusu mtu anayesafiri kwenye muda na kuja kuwasimulia wenzake yale aliyoona kwenye siku zijazo.

👉1
Msafiri Muda (Time Traveller) alikuwa anawaelezea watu kuhusu dhana ya muda. Watu hao walikuwa ni Filby, mtu wa tiba, meya, mwanasaikolojia, msimuliaji na kijana mwingine mdogo.
Msafiri muda anawaambia dhana waliyofundishwa kwenye hesabu kwamba kitu kina vipimo vitatu, yaani urefu, upana na kimo siyo sahihi.
Anawaeleza kila kitu kina vipimo vinne, vitatu ni hivyo vya urefu, upana na kimo na kipimo cha nne ni cha muda.
Anawaeleza kwamba watu wamekuwa hawaelewi dhana ya kipimo cha muda kwenye vitu.
Watu hao wanamweleza mtu anaweza kutembea kwenye vipimo vitatu, lakini ni vigumu kutembea kwenye kipimo cha nne.
Msafiri anawauliza wana uhakika gani mtu anaweza kutembea kwenye vipimo vitatu? Mtu anaweza kwenda mbele na nyuma, kushoto na kulia. Lakini kwenda juu na chini, kuna ukomo kutokana nguvu ya mvutano.
Wanamwambia lakini yapo maparachuti ya kwenda juu, anajibu ni kwa muda tu.
Msafiri anawaambia maisha yetu yote, tangu tunazaliwa mpaka tunakufa, tunatembea kwenye muda.
Anaeleza pale tunapokumbuka tukio fulani la muda na kujiona kabisa tukiwa kwenye tukio lile ni kusafiri kwenye muda.
Hivyo japo watu hawaelewi, wamekuwa wakisafiri kwenye muda miaka yao yote.
Anawaonesha mashine aliyoigundua ambayo inamwezesha mtu kusafiri kwenye muda, wanamkatalia kwamba haiwezekani.
Wanamwambia yaani mtu arudi miaka mingi iliyopita na kushuhudia tukio kama lilivyotokea?
Wanaona ni vigumu.
Anaitoa mashine yake ya muda, ambayo ina ukubwa wa saa na kuwaambia wataijaribu mashine hiyo.
Anaonesha sehemu ambayo mashine hiyo ikibonyezwa itapotea na kisha kumtaka mwanasaikolojia ndiyo aibonyeze ili wasidhani kuna mchezo anawachezea.
Mwanasaikolojia anaibonyeza mashine na inapotea.
Wote wanastaajabu, ila bado wanajiuliza watajuaje imesafiri kwenye muda na hata kama imesafiri, je imerudi nyuma kwenye muda uliopita au imeenda mbele kwenye muda ujao?
Msafiri muda anawapeleka kwenye maabara yake kuwaonesha mashine nyingine za muda alizonazo.

👉2
Walioshuhudia mashine ya muda bado wana maswali mengi na mambo mengi hawayaamini.
Msafiri anawaambia watakutana tena wiki inayofuata kujadili hilo kwa kina na kuwapa uthibitisho zaidi.
Siku ya kukutana inafika, msimuliaji anaenda eneo la kukutana na kuwakuta wengine wawili waliokuwepo wiki iliyopita, mwanasaikolojia na mtu wa tiba, huku kukiwa na wengine wapya watatu, wawili waandishi na mmoja mkimya ambaye hakuzungumza chochote.
Msafiri muda hayupo, ila ameacha maagizo kwamba kama saa moja itafika na hajarudi basi waendelee kupata chakula na atawakuta.
Saa moja inafika, msafiri hajarudi, wanaenda kwenye eneo la kula na kuagiza vyakula. Wakiwa pale mlango unafunguliwa, kuangalia wanamuona msafiri akionekana kuchoka na nguo zake zimechafuka.

Anawasogelea na wanamuuliza kama kila kitu kiko sawa, anawajibu yuko sawa, ila kwanza ataenda kujisafisha kisha apate chakula ndiyo waongee.
Anaondoka na kuwaacha pale na wanaanza kubishana iwapo kwenye mtu huyo huwa anasafiri kwenye muda au ni tapeli tu. Wanajiuliza kama ametoka kwenye safari ya muda ujao, je hakuna namna ya mtu kujisafisha huko mpaka arudi akiwa mchafu.
Wanaendelea kula, msafiri anarudi na wanamwambia awaeleze alipokuwa. Anawaambia hatawaeleza mpaka kwanza ale ashibe. Anawaambia kwa masaa matatu yaliyopita ameishi kwa siku nane, hivyo amechoka sana na pia ana njaa.
Anakula chakula na kumaliza na kuwaambia maelezo ni marefu, waende kwenye chumba kingine.
Wanapofika pale mwandishi anaanza kumwuliza kama ni kweli anasafiri kwenye muda au anatumia ujanja tu kuwahadaa.
Msafiri muda anawaambia anaweza kuwaeleza alikotoka, ila hayupo tayari kubishana nao, hivyo kama wapo tayari wasikilize bila kukatisha. Maelezo ni marefu na yanaweza kuonekana ni uongo, ila anawahakikishia ni kweli kabisa.
Wanakubaliana na masharti yake na anaanza kuwaeleza.

👉3
Msafiri muda anawaambia tangu walipoachana, mashine haikutengamaa kwa muda aliotegemea.
Ni siku hiyo wanayokutana tena asubuhi ndiyo mashine imetengamaa na akaamua kuijaribu.
Anaeleza mwanzo alikuwa na hofu maana haina tofauti na mtu anayejipiga bastola.
Ila alijipa ujasiri, akaingia kwenye mashine na kuiwasha kuelekea muda ujao.
Iliondoka eneo lile kwa haraka na aliona kila kitu kinarudi nyuma.
Alijiona yuko kwenye eneo lenye mawingu na ukungu mkubwa mpaka unaomlowesha.
Aliona majengo mbalimbali ambayo hakuyaelewa, alitaka azime mashine ili kurudi ila akajipa moyo na kuendelea.
Anakutana na kiumbe wa ajabu, kiumbe ambaye anafanana na mtu, ila ana urefu wa futi nne na miguu yake ikiwa peku na alionekana dhaifu.

👉4
Anakutana uso kwa uso na kiumbe huyo, ambaye anageuka na kuongea na wenzake wawili walioambatana pamoja.
Viumbe wale wanajaribu kumsemesha kwa lugha ambayo haielewi, wanaongezeka wengine zaidi na kuonekana kumshangaa yeye na mashine yake.
Walitaka kuigusa mashine yake akawazuia.
Alitegemea watu hao wa miaka ijayo wawe na akili na uwezo mkubwa, lakini alichoona ni tofauti, akili zao ni kama za watoto na miili yao ni dhaifu sana.
Msafiri muda anaona anaweza kuwaua hata kumi kwa kofi moja.
Anaongozana nao ambapo wanaelekea kwenye jengo kubwa, wanaingia ndani ya jengo hilo ambalo limechoka na kuharibika, halijafanyiwa matengenezo kwa muda.
Wanaanza kula, chakula pekee wanachokula ni matunda, ambayo yapo ya kila aina. Anagundua hawali nyama kabisa, kwani katika enzi hizo wanyama kama mbuzi, ng'ombe, kondoo na wengineo wameshatoweka duniani.
Mwanzo msafiri anashindwa kula lakini njaa inapomzidi inamfanya aweze kula matunda hayo.
Anajaribu kuwasiliana nao kwa alama na kuona kwenye hayo matunda wanayokula ni sehemu nzuri ya kujifunza lugha yao. Hivyo anawauliza maswali mbalimbali. Wanamjibu baadhi, lakini baada ya muda wanamuacha na kuondoka.
Kingine kikubwa ambacho msafiri anagundua ni watu hao wanachoka sana haraka. Hawawezi kufanya kitu kimoja kwa muda mrefu.
Anaangalia mashine yake huo ni mwaka gani, mashine inasoma ni mwaka 802701 baada ya kristo na mabadiliko yaliyotokea duniani ni makubwa mno.
Anazunguka maeneo mbalimbali na haoni nyumba za watu, badala yake anaona majengo makubwa

ambayo watu wanakaa kwa pamoja na majengo hayo ni chakavu sana.
Anajiuliza nini kitakuwa kimeipata dunia katika kipindi hicho na wazo linamjia kwamba ni ukomunisti. Kwamba dunia imefikia kuishi kwa ukomunisti katika kipindi hicho, hivyo mambo yote yanafanywa na watu pamoja na hakuna kitu cha mtu binafsi.
Anazidi kuzunguka na anachoona ni bustani kubwa zenye matunda, hakuna mashamba yaliyolimwa, hakuna maduka ya biashara na hakuna kazi yoyote ambayo watu wanafanya zaidi ya kuchuma matunda na kula.
Hata kuzaliana hakupo kwa kiwango kikubwa.
Hiyo inamfanya aelewe kwa nini watu hao ni dhaifu na wasio na akili. Kwa kuwa magumu ya dunia yameondolewa, nguvu walizokuwa nazo watu hazikuwa na matumizi tena na wale watu dhaifu ambao ugumu wa dunia uliwaondoa kabla hawajafika mbali na kuzaliana, walipata nafasi ya kuishi muda mrefu na hivyo kuzalisha watu dhaifu zaidi na zaidi.
Hivyo kilichotokea nu dunia iliyojaa watu dhaifu na wasioweza kufanya chochote.
Msafiri anaeleza kwamba uimara huwa unatokana na mahitaji na usalama huzalisha udhaifu. Hivyo kwa kuwa katika kipindi hicho hakuna uhitaji na usalama ni mkubwa, watu wamekuwa dhaifu mno.
Anaeleza kilichotokea ni asili kujibu kile ambacho wanadamu wamekitengeneza kwa muda mrefu.
Kwa kifupi, maendeleo yote ya binadamu yamesimama na hata yale ambayo yalikuwa yameshafanyika yanaharibika kwa kuwa hakuna matengenezo yanayofanyika.
Akiwa amesimama kwenye mlima na kuangalia jinsi dunia ilivyodumaa, msafiri anajiambia ameweza kuelewa kwa kina tatizo kubwa ambalo dunia ya sasa inalitengeneza ambalo litaipeleka kwenye yale aliyoona kwenye wakati ujao.

👉5
Msafiri muda anaendelea kuelezea kwamba aliendelea kutembea ili kuangalia mazingira ya wakati huo ujao.
Anazidi kuona jinsi ambavyo watu wa wakati huo hawafanyi kazi yoyote, wao ni kulala, kuamka, kucheza, kula, kufanya mapenzi na kulala.
Hakuna kazi yoyote ya kutumia nguvu wanayofanya na hata majengo makubwa yaliyopo, hakuna matengenezo yoyote yanayofanyika.
Msafiri muda anarudi alipoacha mashine yale ya muda anakuta haipo, anapatwa na taharuki, anazunguka kila mahali kuutafuta lakini haipati. Anawauliza watu wale lakini hawamjibu chochote, sana sana wanamshangaa kwa alivyopatwa na taharuki.
Anafika mahali palipofungwa na kuhisi mashine yake imefungiwa huko. Anajaribu kufungua hawezi, anawataka watu wale wamfungulie hawafanyi hivyo. Anatumia nguvu kuvunja lakini pia hafanikiwi.
Anaona huo ni ujinga, kutaharuki hakutairudisha mashine yake zaidi ya kupoteza nguvu zake.
Hivyo anajiambia awe mpole na aitafute mashine taratibu na kama hataipata atengeneze nyingine.
Masaa 24 yamepita tangu amekuwa na taharuki ya kutafuta mashine, amechoka sana na sasa anaamua kuitafuta taratibu na kuonesha ushirikiano kwa watu wale.
Mchana wakiwa wanaogelea kwenye mto, anamuona mmoja akiwa anachukuliwa na maji, huku wengine wakiwa hawahangaiki naye.
Anaingia kwenye maji hayo na kumuokoa, anazidi kuona jinsi viumbe hao walivyo dhaifu kiasi kwamba mawimbi ya kawaida ya maji yanatosha kuwasomba, huku wengine wakiwa hawawezi kusaidia.
Mtu aliyemuokoa ni mwanamke na wanaanza kujenga ukaribu. Mwanamke huyo anampenda na kutaka kumfuata kila mtu, ila tatizo anachoka haraka hivyo mara nyingi alikuwa anamuacha.
Aliona hiyo ni fursa nzuri ya kuipata mashine yake. Anagundua japo watu hao hawaonekani kuhofia chochote, ila wanahofia sana giza na kitu chochote cheusi. Ndiyo maana hawathubutu kulala mmoja mmoja, wanalala kwa pamoja.
Siku moja akiwa na mwanamke huyo anatokea kiumbe mwingine anayefanana na mtu, ila huyu ni mkubwa na mwenye nguvu sana. Kiumbe huyo ametokea chini ya ardhi ambapo yanaonekana ndiyo makazi yake.

Msafiri muda anapata tafsiri nyingine kwamba kwenye miaka hiyo ijayo, jamii ya binadamu itakuwa imegawanyika kwenye makundi mawili, kundi la kwanza ni wale wa juu ambao mazingira yao yanarahisishwa sana kitu kinachowafanya wawe dhaifu.
Na kundi la pili ni wale wa chini, ambao mazingira yao ni magumu, yanapelekea walio dhaifu kubwa na wanaobaki ni wale imara tu.
Hivyo ndivyo ilivyotokea kwa viumbe dhaifu kwenge tabaka la juu na viumbe imara kwenye tabaka la chini.
Msafiri muda pia anapata hisia kwamba ni viumbe hao wa chini ndiyo watakuwa wamechukua mashine yale ya muda.
Anajaribu kumdadisi yule mwanamke aliyejenga naye urafiki kuhusu viumbe hao wa chini lakini mwanamke huyo haoneshi ushirikiano, hataki hata kuwaongelea viumbe hao.

👉6
Msafiri muda anaamua aende chini ya ardhi kutafuta mashine yake.
Yule mwanamke aliyezoeana naye anamzuia asiende, lakini anamuana na kuingia kupitia tundu dogo.
Anaingia na ndani ni giza tupu, hajabeba kitu kitu kingine chochote isipokuwa kiberiti.
Anafika chini na kukutana na viumbe hao wakubwa ambao wanaonekana kuwa na maisha ya tofauti ukilinganisha na viumbe wa juu.
Viumbe hao wa chini wanakula nyama na wanaogopa sana mwanga.
Wanamzingira, anajaribu kuwauliza lakini hawamuelewi, huku wakiongea lugha ambayo haielewi.
Kila anapowasha njiti ili awaone viumbe wanakimbia.
Njiti alizokuwa nazo zinamuishia na kuona anajiweka hatarini.
Anaamua kurudi juu ya ardhi licha ya kujaribu kuzuiwa na kurudishwa na viumbe hao.

👉7
Msafiri muda anaendelea kuelezea kwamba kipindi ambacho kinahofiwa sana na viumbe wa juu ya ardhi ni usiku wa giza, usiku ambao hakuna mwezi.
Hicho ndiyo kipindi ambacho viumbe wa chini ya ardhi hutoka na kuja kuwawinda viumbe wa juu ya ardhi na kuwachukua kama nyama.
Hapa ndipo msafiri anaelewa zaidi kwamba viumbe wa chini ya ardhi huwala wale wa juu ya ardhi.
Pia anaelewa kwa nini hakuwahi kuona makaburi kwa viumbe wa juu ya ardhi.
Hilo linampa hofu kubwa na kutengeneza ulinzi ili naye asikamatwe kama kitoweo.
Anatafuta moto ambao anajua utawakimbiza viumbe hao na bado anaitafuta mashine yake ili aweze kuondoka, akipanga kuondoka na yule mwanamke waliyezoeana.

👉8
Msafiri muda anaendelea kutafuta njia itakayomuweka salama kwa kipindi anachoendelea kutafuta mashine yake ya muda.
Akiwa anaongozana na mwanamke yule rafiki yake, wanaingia kwenye jengo la zamani lenye kumbukumbu za nyuma.
Katika kutafuta anapata kiberiti na chuma, vitu anavyoona ni silaha tosha kwake dhidi ya viumbe wale wa chini ya ardhi.
Anajipanga kukabiliana nao kwa kutumia silaha hizo ili aweze kupata mashine yake ya muda na kuondoka.

👉9
Msafiri muda anaendelea kueleza kwamba aliongozana na mwanamke yule rafiki yake kuelekea mahali ambapo mashine ingekuwepo.
Giza lilipoingia aliona wanaweza kuvuka pori walipo na kwenda kulala juu ya kilima kabla ya kuendelea na safari siku inayofuata.
Lakini ghafla wanasikia sauti za wale viumbe wa ardhini, ni wengi na wamewazunguka.
Msafiri anawasha kiberiti na viumbe hao wanasogea mbali kwa kuona mwanga.

Anakusanya miti na majani makavu ili awashe moto mkubwa. Wakati anahangaika kufanya hivyo, anagundua viumbe hao wamemchukua yule mwanamke.
Moto unawaka mkubwa, msitu unakamata moto na viumbe hao wanaonekana kuhangaika.
Kukiwa na mwanga mkali wanapata upofu, hivyo Msafiri aliwaona wakizunguka zunguka na kuwapiga kwa chuma.
Alimuua mmoja na kuwajeruhi wengine ila baadaye akaamua kuachana nao.
Anamtafuta mwanamke yule ila hamuoni, anafikiria huenda viumbe wale wamemficha mahali ili awe kitoweo kwao baadaye.
Msafiri anajikuta amebaki na chuma na njiti za kiberiti tu, kasha lake hana, limepotea.

👉10
Msafiri muda anaendelea na safari yake ya kuelekea ilipofungiwa mashine, anajisikia kuchoka na usingizi anasinzia mahali.
Baada ya kuamka anafika eneo ilipokuwa imefungiwa mashine.
Kwa mbali anawaona viumbe wale wa juu ya ardhi wakiendelea kucheza na kuogelea kama vile hakuna hatari yoyote.
Anajiuliza jinsi binadamu wamekuwa wanajisumbua na mengi.
Anazidi pia kuona tofauti ya viumbe wa juu ya ardhi na wa chini ya ardhi, mabadiliko, mahitaji na hatari vinawafanya viumbe wa chini kuwa imara kuliko wa juu.
Anasogelea eneo lile na kuchukua chuma yake ili aweze kuvunja, cha kushangaza anakuta pako wazi.
Anatupa chuma aliyokuwa amebeba na kuingia, anaikuta mashine yake ya muda.
Anaenda kwenye mashine na kuanza kuweka nyenzo zake ili aweze kuondoka, ghafla viumbe wale wa chini ya ardhi wanatokea na kumzingira, hana silaha ya kupambana nao.
Anakazana kuweka nyenzo kwenye mashine na kufanikiwa kuondoka.

👉11
Katika kuweka nyenzo za mashine, msafiri muda anakosea na kuweka muda wa mbele zaidi, hivyo mashine inampeleka mamilioni ya miaka mbele.
Kadiri anavyoenda anagundua usiku na mchana vinaenda taratibu sana, mwisho jua dunia inasimama na jua linawaka upande mmoja, huku likififia.
Mwanzo anawaona kaa wakubwa wa baharini na hakuna viumbe wengine.
Lakini kadiri muda unavyokwenda, hakuna viumbe wengine anaowaona.
Mwisho anafika kwenye giza kabisa, ambapo jua limezima kabisa na baridi ni kali.
Anajisikia vibaya na haraka anarudisha mashine yake nyuma.

👉12
Msafiri muda anamalizia kuwasimulia kwamba hivyo ndivyo alivyoweza kusafiri kwenye muda na kurudi. Anajikita yuko kwenye maabara yake kama alivyoondoka.
Anasema mwanzo alikuwa haamini kama ni kweli, alidhani yuko ndotoni, lakini baada ya kuikagua mashine na kujikuta ana maua mfukoni aliyopewa na yule mwanamke aliyemuokoa, anaamini kweli amesafiri kwenye muda.
Anawaambia kwamba atawaelewa kama hawatamuamini, wanaweza kusema ni ndoto zake au amekuwa akifikiria sana kuhusu kesho ya wanadamu na akili yake kumtengenezea picha hiyo.
Lakini yeye anachojua ni amesafiri kwenye muda.
Waliokuwa wanamsikiliza hawaonekani kumwamini, wanamuuliza maswali mbalimbali kisha wanaondoka.
Siku inayofuata msimuliaji anarudi kwa msafiri muda, anaambiwa yuko maabara. Anaenda maabara hamkuti, ila mashine ipo. Muda mfupi baadaye msafiri muda anakuja akiwa amebeba kamera na kumwambia atasafiri tena kwenye muda na kurudi na ushahidi wa picha.
Msimuliaji anamuona msafiri muda akiondoka na mashine ya muda, ila miaka mitatu baadaye bado hajarudi.
Anashindwa kuelewa iwapo msafiri alienda muda ujao au uliopita na kama amekwama kwa kuchagua

kubaki au amekwamishwa.
Lakini kwa vyovyote vile, ni vyema kuishi vizuri kwenye wakati tulionao.

👉SOMO
Riwaya hii inatufundisha mengi sana kuhusu mwenendo wa dunia na yale yatakayotokea iwapo mambo yataenda kama yanavyoenda sasa.
Tumekuwa tunaona juhudi mbalimbali za kiserikali na kijamii kutaka kurahisisha maisha ya kila mtu.
Mfano mifumo ya uchumi ya ujamaa na ukomunisti inahubiri sana watu kupewa kila kilicho muhimu bila hata ya kufanya kazi.
Matokeo yake ni kuishia kutengeneza kizazi cha watu dhaifu ambao hawawezi hata kupambana na changamoto za asili.
Hatupaswi kutaka mambo yawe rahisi, bali tunapaswa kuwa imara kuweza kukabiliana na chochote.
Kadiri mambo yanavyokuwa magumu, ndivyo na sisi tunapambana kuwa imara kukabiliana nayo.
Asili huwa inatupa njia za kukabiliana na chochote tunachokutana nacho, tunapokwenda kinyume na asili, lazima tulipe gharama kubwa.
Kwenye maisha, pambana kuwa imara badala ya kutaka mambo yawe rahisi.

Muhtasari huu umeandaliwa na Kocha Dr Makirita Amani,
www.t.me/somavitabutanzania